

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



09 FEBRUARI, 2018



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI

KIKAO CHA TISA – TAREHE 09 FEBRUARI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Mwaka ya Upimaji wa Utekelezaji wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kwa Mwaka 2016/2017 [Annual Performance Evaluation Report on Public Procurement Regulatory Authority for Financial Year 2016/2017].

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **108. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga ambao umeanzishwa kwa nguvu za Wananchi.

##### **109. MHESHIMIWA PROF. NORMAN ADAMSON SIGALLA KING (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mwaka 2013 Serikali ilianza kutekeleza mradi wa maji wa Kata za Kinyika na Matamba katika Wilaya ya Makete lakini mradi huo haukufanikiwa kutokana na Serikali kutoa maelekezo ya kulaza mabomba ya inchi 2.5 na 4 badala ya 8 kwenye mradi wa km 18; na mradi wa maji wa Tarafa za Magoma na Bulongwa ulijengwa muda mrefu wakati idadi ya watu ikiwa ndogo lakini sasa idadi ya watu na matumizi vimeongezeka:-

- (a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Tarafa ya Matamba;
- (b) Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa Tarafa ya Bulongwa ili Kata za Bulongwa, Kipagalo na Lawumbu ziweze kupata maji.

#### **110. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):-**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kwa muda mrefu wananchi wa Karagwe wamekuwa wakiahidiwa kujengewa Hospitali ya Wilaya; na taratibu zote zimekuwa zikifuatwa kupitia vikao vya Baraza la Madiwani na RCC lakini maombi haya hutupiliwa mbali na TAMISEMI:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali hii ambayo pia ipo kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais.

#### **OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

#### **111. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini mfumo wa EPICOR, LGMD na ule wa LAWSON iliyopo kwenye Halmashauri itaanza kuwasiliana na siyo kuwa “*stand alone system*” kama ilivyo sasa.

### **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

#### **112. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMMED ISSA (MTAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Kwa takwimu zilizopo inakisiwa kuwa watu wote wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania ni zaidi ya milioni moja na laki tano na inaaminika kuwa Wanawake ndio waathirika wakubwa zaidi ikilinganishwa na Wanaume:-

Je, ni sababu gani za kitaalamu ambazo zimesababisha Wanawake kuwa ni waathirika zaidi kuliko Wanaume.

#### **113. MHESHIMIWA KITETO ZAWADI KOSHUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Vifo vya mama na mtoto katika Mkoa wa Mwanza

pamoja na mambo mengine huchangiwa na kukosa huduma za upasuaji, damu salama na upungufu wa watumishi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza vifo vyaa mama na mtoto.

### **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

#### **114. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

- (a) Je, kuna Sheria yoyote ya nchi inayomruhusu Askari Polisi kumkamata mtuhumiwa, kumpiga na kumtesa kabla hajajua kosa lake na kabla ya kufikishwa katika Kituo cha Polisi;
- (b) Je, Serikali inachukua hatua zipi za kuhakikisha kuwa Askari wanaofanya vitendo kama hivyo wanawajibishwa kwa mujibu wa Sheria za nchi;
- (c) Je, mpaka sasa ni Askari wangapi wameshachukuliwa hatua za Kisheria kutokana na makosa ya kujichukulia hatua mkononi.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**115. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Wananchi wa Wilaya ya Chunya wameanza kujenga uwanja wa michezo wa kisasa wa Wilaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi huo ukamilike haraka.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**116. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Wanawake wengi bado hawaelewi haki zao hasa kuhusu haki za kumiliki ardhi:-

Je, kuna mkakati gani wa Serikali wa kuwawezesha wanawake waweze kujua haki zao za kumiliki ardhi.

## **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

### **117. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mwaka 2014/15 Serikali iliahidi kuongeza usambazaji maji katika Vijiji 100 vilivyoko umbali wa km12 kutoka Bomba Kuu la Ziwa Victoria hadi Kahama na Shinyanga na Serikali ilishatenga shilingi bilioni 4 ili kutekeleza mradi huo:-

- (a) Je, Vijiji vingapi vimeshapatiwa maji kati ya hivyo 100 hadi sasa;
- (b) Je, Serikali itafikisha lini maji ya Ziwa Victoria katika Vijiji vya Mwakazuka, Mwaningi, Kabondo, Ntundu, Busangi, Buchambaga, Nyamigege, Gula, Izuga, Buluma, Matinje na Bubungu.

## **WIZARA YA MADINI:**

### **118. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Katika Ukanda wa Bonde la Ziwa Rukwa katika Jimbo la Kwela, kwenye ukingo wa Milima ya Lyamba,

Lyamfipa inayoambaa katika Kata za Mfinga, Mwadui, Kalumbaleza, Nankanga, Kapeta hadi Kaoze, baadhi ya Wananchi wamekuwa wakiokota madini mbalimbali bila kutambua ni madini ya aina gani:-

- (a) Je, Serikali imeshafanya utafiti wowote katika maeneo hayo;
- (b) Kama jibu ni hapana Je, ni lini itafanya utafiti ili kujua eneo hilo lina madini ya aina gani.

#### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

#### **119. MHESHIMIWA JOYCE BITA SOKOMBI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:- Kwenye Bahari na Maziwa yetu kuna samaki wa aina mbalimbali kama vile dagaa, fuvu, uchuvi au dagaa mchele na wengine ambao ni wadogo sana:-

- (a) Je, ni nyavi zenyetukubwa wa saizi gani zinahitajika kwa ajili ya uvubi wa aina hizo ndogo ndogo za samaki;
- (b) Je, Serikali inafanya utaratibu gani wa kuwapatia wavuvi wa aina hiyo ya samaki nyavyu zinazohitajika;

(c) Je, elimu ya kutosha kwa nyavu husika imefanyika kwa kiwango gani hasa kwa wavuvi wanaozunguka Ziwa Victoria.

### **WIZARA YA NISHATI:**

#### **120. MHESHIMIWA OMARY TEBWETAN MGUMBA (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kata sita za Tegetelo, Kibuko, Tomondo, Tununguo, Serege, Matuli na Mkulazi katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki hazijafikiwa na miundombinu ya umeme mpaka sasa:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata hizo.

### **IV. HOJA ZA KAMATI:**

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

### **V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**

•

### **VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU:**



### **VII. WIMBO WA TAIFA:**

**DODOMA**  
**09 FEBRUARI, 2018**

**S.N. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**